**HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI**
**SHULE YA SEKONDARI MACHOCHWE**
**S.L.P 164, MUGUMU - SERENGETI**
**SIMU: +255 756086285 AU +255767083823**

**KUMB NA: MSS/INST/VOL 2/2021**

MWANAFUNZI.................................................
.................................................

YAH:**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI MACHOCHWE WILAYA YA SERENGETI MKOA WA MARA MWAKA 2021.**

**1.0:UTANGULIZI**

Ninafurahi kakuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Machochwe kwa mwaka wa masomo 2021. Shule ya sekondari Machochwe ipo umbali wa Km 22 Mashariki mwa mji Mkuu wa Wilaya (Mugumu) – Halmashauri ya wilaya ya Serengeti.

Muhula wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti shuleni siku hiyo saa 1:00 asubuhi ofisini kwa Makamu Mkuu wa Shule kwa wale wanafunzi wa bweni wanatakiwa kuripoti tarehe 10/01/2021. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 20/01/2021 baada ya hapo utahesabika mtoro na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yako ikiwa ni pamoja na fursa hii kufutwa.

HEADMASTER
MACHOCHWE SECONDARY SCHOOL
MUGUMU

2.0: **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2:1: SARE YA SHULE**

**A. WAVULANA**

I. Suruali mbili (02) za rangi ya dark blue nzito. Suruali iwe na marinda mawili kwa mbele na turn-up na **ISIWE YA KUBANA WALA MODO zisiwe za mtumba**. Mashono ni mifuko miwili pembeni na mmoja nyuma, suruali iwe na marinda mawili na upana wa kutosha chini (inchi 18) na ivaliwe kwa heshima daima.

II. Shati mbili nyeupe **Tetroni/TOMATO** mikono mifupi yenye mfuko mmoja kushoto **YAMITUMBA HAIKUBALIKI**.

III. Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba na kisigino kifupi.

IV. Soksi jozi mbili rangi nyeusi.

V. Sweta rangi ya dark blue lenye muundo wa" V" kifuani isiyo na maandishi wala mchoro wowote.

VI. Mkanda mweusi wenye msumari (hook) unaoingia kwenye matundu.

VII. Tai rangi ya dark blue yenye chuma.

**B. WASICHANA**

I. Sketi mbili (02) za rangi ya dark blue nzito zenye linda box kulia na kushoto na mchirizi mweupe mbele na ziwe ndefu zenye kuvuka magoti . **ZISIWE ZA MTUMBA**. Iwe ndefu mpaka chini (**Zingatia maelekezo haya, sketi fupi hutapokelewa) sketi isizidi cm 15 kutoka kwenye mguu.**

II. Shati mbili (02) nyeupe Tetroni/TOMATO mikono mifupi yenye mfuko mmoja kushoto.

III. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na kisigino kifupi.

IV. Soksi jozi mbili (02) rangi nyeupe ndefu zinazofunika misuri.

V. Sweta rangi ya dark blue lenye muundo wa" V" kifuani isiyo na maandishi wala mchoro wowote.

VI. Hijabu ifanane na sare ya shule kwa waislamu.

VII. Tai rangi ya dark blue fupi.

**C. SARE ZA MICHEZO**

I. T-shirt rangi ya kijani isiyo na maandishi yoyote.

II. Raba na soksi ndefu.

III. Track suti rangi ya kijani (itavaliwa kila ijumaa).

**D. MAHITAJI YA BWENI**

I. Nguo za kushindia, gauni kunguru ya rangi ya kijani (CHEKUCHU) mshono wa solo ndefu.

II. Godoro inchi **TATU KWA SITA** (3X6) , shuka mbili (02) za rangi ya blue bahari au pink, Net ya mbu, na **blanket**

III. **VYOMBO VYA CHAKULA**: sahani, kikombe na kijiko

IV. Beseni na ndoo

V. Atatakiwa kuwa na **SOFT BROOM** kwa ajili ya usafi chumbani kwake.

VI. **MATIBABU NI JUU YA MZAZI/MLEZI MWENYEWE** kama mwanao hana Bima ya Afya unashauriwa kumkatia CHF Au aje na TSH 5000/= kwa ajili ya kukatiwa Bima hiyo

HEADMASTER
MACHOCHWE SECONDARY SCHOOL
MUGUMU

**3:0.VIFAA VYA KUJIFUNZIA**

I. Dictionary
II. Mathematical set.
III. Madaftari makubwa COUNTER BOOK yasiyopungua kumi (10).
IV. Rula ya sentimita thelathini.
V. **Ream paper moja (karatasi nyeupe) uje nayo siku ya kuripoti.**
VI. **Kiti na meza(Fremu ya chuma).mchoro umeambatanishwa**

**4:0. VIFAA VYA USAFI NA MAZINGIRA**

I. Kwanja
II. Chelewa la kufagilia
III. KILA MWANAFUNZI AJE NA MCHE MMOJA WA MTI ATAUTUNZA HADI ATAKAPO MALIZA KIDATO CHA NNE NA KUUKABIDHI.

HEADMASTER
MACHOCHWE SECONDARY SCHOOL
MUGUMU

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mjibu wa sheria ya elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha , inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo Ufundi yenye dhamana na Elimu Nchini na Ofisi ya Rais- TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara ufikapo shuleni.

I. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na wanajamii kwa ujumla.
II. Mahudhurio mazuri katika shughuli za ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
III. Kushiriki kwa umakini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
IV. Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
V. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
VI. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
VII. Kuvaa sare ya shule wakati wote wa unapotakiwa.
VIII. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
IX. Kutunza mali ya umma.

## MAMBO AMBAYO MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUFANYA.

I. Kuvuta Sigara
II. Kufuga ndevu
III. Kufuga nywele
IV. Kufuga kucha ndefu
V. Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima
VI. Kugombana
VII. Kuiga mitindo ya kihuni kwa kunyoa kipara kupaka kucha rangi n.k
VIII. Kujichubua ngozi ya mwili kwa kutumia madawa
IX. Kuja shuleni bila kuvaa sare ya shule
X. Kuvaa kofia, bangili na mapambo mengine yeyote akiwa shuleni
XI. Kutembelea sehemu zifuatazo (isipokuwa kwa kibali maalumu)
    - Chumba cha walimu (staff room)
    - Ofisi ya mkuu wa shule
    - Maabara
    - Jikoni
    - Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu
    - Vilabu vya pombe
    - Majumba ya starehe
    - Majumba ya kufikia wageni

HEADMASTER
MACHOCHWE SECONDARY SCHOOL
MUGUMU

**MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA**

I. WIZI
II. Uasherati /ubakaji na ushoga
III. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
IV. Uvutaji wa bangi
V. Makosa ya jinai
VI. Kupiga au kupigana
VII. Kugoma au kuchochea fujo au kuongoza mgomo au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
VIII. Kudharau Bendera ya Taifa
IX. Kuoa au kuolewa
X. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani nan je ya shule
XI. Kutoa mimba
XII. Kugomea adhabu kwa makusudi.
XIII. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
XIV. Mwanafunzi Kuwa na simu ya mkononi.

**Tanbihi: "SHULE HAITAMVUMILIA MWANAFUNZI YEYOTE MWENYE UTOVU WA NIDHAMU"**

**5.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULE NA MWANAFUNZI**

A. Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospital ya serikali Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara tu utakaporipoti shuleni.
B. Fomu ya maelezo binafsi ya kuhusu historia ya mwanafunzi mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
C. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule
D. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

………………………………………………..

RAMADHAN OWADE ODINDO

HEADMASTER
MACHOCHWE SECONDARY SCHOOL
MUGUMU

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI MACHOCHWE**

**HISTORIA/TAARIFA YA MWANAFUNZI.**

1. JINA LA KWANZA……………………………… JINA LA KATI………………………
   JINA LA UKOO…………………………………………
2. JINA LA MZAZI/ MLEZI………………………………………………………………………
3. KAMA NI MLEZI TAJA UHUSIANO……………………. MF (KAKA,MJOMBA,N.K) NAMBA YA SIMU YA MZAZI /MLEZI ……………………………………………..
4. ANUANI YA KUDUMU YA MZAZI/MLEZI……………………………………………
5. MAHALI MWANAFUNZI ALIPOZALIWA KIJIJI CHA……………………………….KATA YA ………………… WILAYA YA………………………MKOA WA………………………..
6. DINI…………………………………
   DHEHEBU……………………………………………
7. UNAINGIA KIDATO CHA ……………………….. TAREHE……………………………
8. KUTOKA SHULE YA MSINGI /SEKONDARI……WILAYA…………………MKOA…
9. MZAZI /MLEZI WAKO ANAFANYA KAZI YA AJIRA/MKULIMA/BIASHARA ……………………………………………………………MAHALI …………………………..…
10. NDUGU WENGINE AMBAO WANAWEZA KUPELEKEWA HABARI MUHIMU JUU YAKO/MASUALA YA SHULENI NI
    I. ……………………………………………………UHUSIANO……………… ………
       NA SIMU………………………
    II. ………………………………………………UHUSIANO………………… ………
       NA SIMU ……………………
11. KABLA YA KUJA HAPA SHULENI UMEPIMWA NA DAKTARI? NDIYO/HAPANA. NI UGONJWA UPI WA KUDUMU KWAKO?.........................................................................................
12. SIFA MAALUMU KAMA UNAZO…………………………………………………………
13. TAARIFA ZA WAZAZI: WAPO (     ) WAMEFARIKI (    ) WEKA VEMA PANAPOHUSIKA
    NAKILI KUWA MAELEZO NILIYOYATOA HAPO JUU NI SAHIHI

……………………. ……………………

SAINI YA MWANAFUNZI SAINI YA MZAZI/MLEZI

***MUHIMU: BAADA YA KUJAZA FOMU HII IREJESHWE SHULENI WAKATI WA KURIPOTI***

HEADMASTER
MACHOCHWE SECONDARY SCHOOL
MUGUMU

MEDICAL EXAMINATION **FORM**

PRESEDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT.

MACHOCHWE SECONDARY SCHOOL

P.O.BOX 164

MUGUMU-SERENGETI

.........................................

TO MEDICAL –OFFICER

......................................................................................

......................................................................................

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF A STUDENT

SELECTED TO JOIN FORM................................ YEAR...........................................

NAME OF PUPIL/STUDENT.......................................................................

**P**lease examine the above mentioned as to his/her fitness for Secondary School Education according to following items below

| NO | ITEM | CONDITION | REMARKS |
|---|---|---|---|
| 1 | Mental condition | | |
| 2 | Sight | | |
| 3 | Hearing | | |
| 4 | Chest T.B | | |
| 5 | Urine | | |
| 6 | Stool | | |
| 7 | Nose | | |
| 8 | Blood pressure | | |
| 9 | Pregnancy (for Girls) | | |
| 10 | Blood Group | | |
| 11 | H.B | | |

Any other physical disability not listed that may affect his/her studies

...................................................................................................................

...................................................................................................................

Name.........................Signature............................DATE..................

**MEDICAL OFFICER OFFICIAL STAMP**

HEADMASTER
MACHOCHWE SECONDARY SCHOOL
MUGUMU

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE
(IJAZWE NA MWANAFUNZI NA MZAZI)

Mimi……………………………………………………………………………mtoto wa (baba)……………...........................Mama……..………………niliyezaliwa tarehe……mwezi wa ……mwaka………na kuhitimu elimu ya msingi katika shule ya msingi ya………………......naishi katika kijiji cha…………………………………………
Nimezisoma sheria za shule, kanuni na taratibu za shule mbele ya mzazi/mlezi wangu. Naahidi kuwa nitakuwa mtiifu kwa uongozi wa shule na nitazingatia kanuni na taratibu zote kama zilivyoainishwa na kwamba sitashiriki katika vitendo vyovyote viovu kama migomo, fujo au makosa ya jinai. Nitaripoti shuleni na kuanza masomo kwa tarehe zilizopangwa wakati wote nikiwa na vifaa na mahitaji yote ya shule na naahidi kusoma kwa bidii.

JINA LA MWANAFUNZI………………………………………………………………

SAINI…………………………

FOMU YA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI
(IJAZWE NA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI)

Mimi……………………………………………………wa kata ya…………………

Kijiji cha…………………………ambae ni mzazi/mlezi wa…………………………..

Naahidi kuwa nitashirikiana na Uongozi wa shule kusimamia Malezi bora ya mwanangu kwa kuhakikisha kwamba anazingati sheria,kanuni na taratibu za shule na kwamba nitamlipia/mnunulia mwanangu mahitaji yote muhimu ya shule kwa wakati.


JINA LA MZAZI/ MLEZI……………………………………………………………


SAINI………………………………………

***MUHIMU: BAADA YA KUJAZA FOMU HII IREJESHWE SHULENI WAKATI WA KURIPOTI***

HEADMASTER
MACHOCHWE SECONDARY SCHOOL
MUGUMU

# VIPIMO VYA KITI NA MEZA




HEADMASTER
MACHOCHWE SECONDARY SCHOOL
MUGUMU